



**Kuwatunza
Watoto**
Namna za
kukuza watoto
nchini Australia

Shirika la Kuwatumza watoto

limeandikwa ili kuwasaidia wazazi ambao wanaishi Australia, kuwawezesha kutunza familia zao kuwa na nguvu, furaha pia afya bora.

Kuwatumza watoto inaweza kuwa vigumu. Kwa wazazi ambao wamekuja Australia kutokea nje, kuna shinikizo kubwa ambalo limewekwa juu ya utunzaji wa watoto ndani ya nchi mpya na mazingira mapya ya kitamaduni.

Watoto, kupitia shule na shughuli zingine, mara nyingi inakuwa rahisi kujifunza mila, lugha na desturi za Australia kuliko wazazi wao.

Kitini hiki kitawasaidia wazazi kutunza familia zao [nchini Australia] na jinsi [ya] kupata msaada kipindi unapohitajika nchini Australia.

Kuwatumza Watoto hutoa taarifa kuhusu:

- **Namna ya ukuaji wa watoto**
- **Namna ya kuwasiliana na watoto**
- **Jinsi ya kuwakuza vijana kwenye utamaduni mpya**
- **Kuwaacha watoto nyumbani peke yao wakiwa salama.**
- **Namna ya kutoa adabu kwa watoto**
- **Namna ya kuwatumza watoto salama**
- **Mahali pa kupata ushauri na msaada.**

Kitini hiki kimetolewa kwa ajili ya wazazi pia ni chanzo kwa ajili ya mijadala kwa wafanya kazi juu ya mada hizi wakiwa na wazazi kama sehemu ya kazi za makundi na eneo la kujadiliwa.

Kinapatikana kwa Kiingereza, Kiarabu, Kifarsi, Kitamili, Kiswahili na Kidinka kwenye: ssi.org.au/resources/publications.

Shukrani za pekee kwa Victoria Smith na Elizabeth Schaffer kwa mchango wao katika kuandaa kijitabu hiki.

Kuwatumza watoto imefadhiliwa na Familia na Huduma za kijamii chini ya Mpango wa *Kuwafanya Waendeleo kuwa Salama*.

Funded by the



Namna watoto wetu wanavyokuwa

Tangu wanapozaliwa, watoto wetu hukua pia huanza kuonesha mabadiliko. Kila mtoto ni tofauti; baadhi yao hukua kwa haraka, na baadhi hukua taratibu. Wazazi hupenda kufahamu jinsi watoto wanavyokua kwa afya na furaha pia kujifunza kwa kadili wakuavyo. Orodha hii ni muongozo wa njia za kawaida za ukuaji na mabadiliko ya watoto.

Miezi 0–6

Katika miezi 6 ya mwanzo watoto wachanga hupenda kubebwa na kukumbatiwa kiukaribu zaidi. Hufanya mawasiliano kwa kulia. Kwa kadili wakuavyo, hulia kwa njia tofauti kwa kuwaambia wazazi kitu gani wanakihitaji – Nina njaa, Nimechoka, Ninaogopa, au Nimejikojelea. Watoto wachanga hujifunza kwa kutazama, kusikiliza na kugusa. Ni vizuri kuwapatia vitu vipya kuvigusa na kuviona. Kuongea, kuimba na kusoma ni vitu vinavyowafurahisha na kuwasaidia kujifunza kuongea. Wasikilizapo sauti za wazazi huwafanya kuwa wakimya na wenye amani.

Miezi 6–12

Kuanzia miezi 6 hadi 12, watoto huhitaji kuzungumza, kuimba, kusoma pamoja na wazazi na wanafamilia. Huwa wanafurahi kwa makelele pindi tu wakigundua kuwa unawaelewa, nao hurudisha tabasamu kwa kicheko cha mazungumzo ya kitoto. Wanafahamu sauti za wanafamilia, huwa wanaona aibu kwa sauti na nyuso ngeni. Huanza kujitokeza, kukaa, kujizungushazungusha na wengine huanza kutambaa na kujaribu kusimama.



Miezi 12 – Miaka 2

Kufikia umri wa miezi 12, watoto wengi huweza kuongea maneno machache na wengine kufikia umri wa miaka 2 huweza kuongea sentensi fupi fupi. Pia watoto wataanza kucheza, pia hujifunza kutembea. Wawe karibu na wanafamilia na kutaka kupata faraja ya kukumbatiwa. Huanza kujifunza kufanya vitu ambavyo wazazi wao wamewaambia wafanye.

Miaka 2–3

Watoto kati ya miaka 2 na 3 hujifunza mambo mengi. Hutaka kukaa karibu na wazazi lakini pia huanza kujionesha kwa wanaowazunguka. Hutaka kufanya mambo bila msaada na wanasema 'hapana' nyingi. Kama hawapati wanachotaka huweza kupiga kelele na mayowe na kupiga miguu yao. Hii hali huwachosha sana wazazi lakini ni ndio asili, na watoto wanahitaji wazazi wao kuwaonyesha upendo na kuwaweka salama.

Miaka 3–5

Kati ya miaka 3 na 5 watoto hupendelea kuzungumza na wao huuliza maswali mengi na kusema 'kwa nini' maswali ni mengi. Huzungumza na kila mtu kwa - familia, marafiki, na hata midoli yao. Wana upendo sana na huanza kujifunza kushirikiana na kuwa na marafiki. Sasa wanaweza kuanza kuelewa mema na mabaya.

Miaka 7–10

Watoto wa miaka kati ya 7-10 hukua kwa haraka, kujifunza mambo mapya na kuwa na marafiki wapya. Hutaka watu wawapende na wanataka kuwa wazuri katika mambo. Kuwasaidia na kuwaongoza katika wakati huu huwasaidia kuwa na ujasiri na mafanikio shuleni.

Miaka 10–12

Mabadiliko ya kimwili ambayo huanza katika umri huu huwafanya watoto kujisikia na hawana raha na aibu. Watoto wengi huanza kujiuliza au kuongelea juu ya imani na maamuzi ya wazazi wao. Hisia zao hubadilika haraka na wanaweza kuonyesha nia ndogo katika familia. Heshima yenye hisia ni muhimu kwa watoto hivyo wazazi huwapaswa kuchukua muda wa kuwasikiliza. Watoto wengi huanza kujawa na wasiwasi kwa namna gani watu wengine wanavyowafikiria hivyo ni muhimu kuwasaidia wajisikie vizuri na kuwa na wenye kujiamini.



Miaka 5–7

Watoto wenye umri kati ya miaka 5 – 7 wapo kamili kimawazo na nguvu; wanafurahia kucheza, kusimuliana hadithi na kufanya mambo mbali mbali. Wanapoanza shule kunahitaji mabadiliko makubwa lakini pia uchovu na kuogopa hivyo wanahitaji uangalizi mkubwa sana kutoka katika familia. Wanataka watu wawapende na kuwafikiria kama wao ni watu wazima, wanaweza kuchukia kirahisi kama watafikiria kuwa watoto wengine si wema kwao. Wanaweza kuwa ni wagumu kwa kufanya kile walichoelekezwa kufanya, hivyo wazazi huwalazimu kuwa na subira.

Miaka 13–19

Hii ndio miaka ya 'ujana' ambayo kijana anakua kutoka utotoni kuwa mtu mzima. Inaweza kuwa ni wakati mzuri au mgumu. Ni kawaida kwa vijana kutaka kutumia muda mwingi na marafiki zao na muda kidogo kwa familia zao. Hujifunza kuwa wao ni akina nani na wanapenda kupata mitindo yao wenyewe ya kuvaa, mitindo ya nywele, muziki, na marafiki. Ni kawaida kwa vijana kuwa na hisia kali - furaha, hasira, na kutotaka kuzungumza. Wazazi wanaweza kuwaongoza, na kuwafundisha tabia zinazokubalika na zisizokubalika, lakini ingefaa kama wanaweza kuwapa uhuru.




Kila mtoto ni tofauti; baadhi yao hukua kwa haraka, na baadhi hukua taratibu.

Kuwasiliana na watoto

Kazi ya wazazi na jamii kwa kila mahali ni huduma kwa watoto, kuwaweka salama, wenye furaha, afya, na nguvu. Wazazi katika nchi na jumuiya mbalimbali huwasiliana na watoto katika njia tofauti tofauti. Mawasiliano mazuri ni pale wazazi na watoto huaminiana na kuheheshimiana.

Namna wazazi wanavyowasiliana na watoto wao hubadilika kwa kadili watoto wanapokua. Siku zote kutakuwa na nyakati ngumu wakati watoto hawataki kufanya ambacho wazazi wanataka au kuwa na maadili ambayo wazazi hawayapendi. Wanapowasiliana vizuri, zaidi ya matatizo haya yanaweza kuepukwa.



Mawasiliano ni njia mbili

Mawasiliano mazuri ni ya kuzungumza na kusikiliza. Wazazi wanaposikiliza kipi watoto wanasema, hujifunza mengi juu [ya] watoto wao na inasaidia watoto kujisikia wajasiri, wenye kuheshimiwa na wenye usalama. Watoto huwasiliana katika njia tofauti tofauti katika umri tofauti lakini watoto wote huhitaji usikivu wako; waache wamaliza kile wanachosema na usijaribu kuwapinga au kuwakosoa.



Ufahamu

Ilivyo rahisi kwa watu wazima kufahamu mara nyingi si rahisi kwa watoto kufahamu. Muda mwingine ambapo watoto wanakuwa hawana adabu, ni kwa sababu hawajaelewa. Kuwauliza maswali na kuwaachia nafasi ya kuelezea vitu kwa maneno yao yaweza kurahisisha. Wakati mwingine tabia mbaya ni ishara ambayo kitu Fulani hakipo sawa na mtoto huyo anahitaji tahadhari ya ziada na kumjali.



Furahia kutumia muda ukiwa na watoto

Kutumia muda ukiwa na watoto na kufanya mambo kwa kuwa nao, hufurahia kwa kujenga uaminifu na mawasiliano mazuri. Kuzungumza na watoto juu ya mambo wanayofurahia kama muziki au michezo na kusikiliza nini wanachotaka kusema. Cheza michezo ukiwa na watoto wako, Tumia muda mwingi pamoja nao na mfurahie.

Watoto uwaambie kuwa umefurahi kuwa nao

Watoto hupenda kujua kuwa wazazi wanafuraha na fahari ya wao, hivyo wafahamu wakati wanakufanya kitu vizuri. Hii huwatia moyo pia hujinyenyekeza kwa wazazi wao na kuongeza na huwafanya wawe wa kujiamini zaidi. Kuwa wenye furaha na kujiamini huwasaidia kujifunza, kuwa na marafiki na kujiheshimu.

Kuwa na sheria za wazi, thabiti na za kuaminika

Ni muhimu kwa watoto kuwa na sheria ambazo wanaweza kuzielewa na kuzifuata. Kanuni hizi lazima ziwe za haki, mantiki na ziendane na umri wa mtoto. Ni vizuri kama sheria hazitabadilika wakati wote lakini pia ni vizuri kwa wazazi kuwa warahisi. Kwa mfano, sheria za kwenda kulala zinaweza kubadilika wakati wa likizo za shule.

Kusaidia watoto kuzungumza

Ni vigumu sana kwa mtoto ambaye ana hofu kuwasiliana na kuwa mwaminifu na mkweli. Kuwachukiza, kuwatukana kwa makelele au kuwatishia kuwadhuru, inawafanya kuwa wagumu sana kuwasiliana. Hata kama unadhani wamekuwa wakolofi, ni vizuri basi kuwapa nafasi watoto kuelezea matendo yao. Kuwasikiliza watoto kunaweza kukusaidia kuelewa wana nini na kwa nini.



Usiwe na hasira

Jitahidi kutokuwa na hasira kwa mambo ambayo watoto wanakuambia. Majibu yako ya hasira yanaweza kuwafanya watoto waache kuzungumza kwa uwazi. Usizungumze na watoto kama una hasira. Tulia kwanza kisha utazungumza nao baadae.



Namna ya kuwakuza vijana kwenye utamaduni mpya

Vijana wenye umri katika ya 13-19 wanaitwa 'vijana'. Huu ndio muda wa kufanya mabadiliko kwa vijana wadogo pamoja na familia zao.

Mabadiliko huwa ni ya kawaida na ya muhimu

Vijana hubadilika kutoka kuwa watoto kwenda utu uzima na wanajifunza mambo mengi mapya. Hupitia na mabadiliko katika miili na hisia zao na katika maisha yao ya kijamii na tabia.

Wazazi wanaweza kuelewa baadhi ya mabadiliko hayo ya kawaida kwa watoto vijana wao, ambapo:

- kuanza kujiona wenyewe kama wametengwa kutoka kwenye familia na kuhitaji usiri zaidi
- hutaka kufanya maamuzi zaidi wenyewe
- hupata maoni tofauti tofauti na mawazo kutoka kwa wazazi
- hupenda kutumia muda mwingi wakiwa na rafiki zao na husikiliza kwa makini katika umri huu.

Wazazi wakati mwingine wanakuwa wasiwasi kwamba watoto wao vijana wana tabia mbaya. Hii inaweza kusababisha migogoro lakini kama wazazi ni wavumilivu wanaweza kutafuta njia mpya ya huduma kwa ajili ya watoto wao wakati wanakuwa katika utu uzima.

Wajue vijana wako

Wazazi wanatakiwa kuwa na taarifa ya kuwa vijana wanafanya nini na wanawaza nini ili kuhakikisha kuwa wako salama na vizuri. Muda mwingi kaa na vijana, fanya mambo wanayopenda na ufahamu wanapendelea nini zaidi ili kudumisha uaminifu.

Zungumza na vijana

Ni muhimu kwa wazazi kuwa na mawasiliano mazuri na vijana wao. Unavyo ongea na kijana ni tofauti na utakavyo ongea na mtoto mdogo. Vijana huanza kuhisi ni wakubwa na huhitaji kuheshimiwa, kwahiyo kujadiliana nao na kuwaweka wazi ni muhimu.

Vijana hubadilika kutoka kuwa watoto kwenda utu uzima na wanajifunza mambo mengi mapya.

**Ni vizuri kuonyesha kwa vitendo
kitu mbele ya vijana kuliko
kuwambia maneno tu.**

Faraja na heshima

Vijana wanahitaji kufarijiwa ili wafanye vitu vizuri na hupenda kusifiwa pale wanapofanya vitu vizuri. Kwahiyo wazazi wana ulazima wa kutunza kumbukumbu kwa yale mazuri yaliyo fanywa na vijana. Pia kuheshimu kile kitu wanacho kifikilia hiyo itawajengea uaminifu na kujiamini.

Uwazi na usawa

Nivigumu kuwalazimisha vijana kufanya vitu ambavyo hawapendi kufanya. Sema 'hapana' au 'utafanya hiki' maana bila kumruhusu kijana kufanya uchaguzi au kutoa maoni yake kunaweza kupelekea ugomvi. Japo ni nzuri kwa wazazi kuweka sheria lakini wanatakiwa wawape uhuru vijana katika kufanya maamuzi yao.

Kwa mfano, kama mzazi anaogopa kijana wake kwenda kwenye tukio fulani na vijana wenzake kwa mara ya kwanza, unaweza kumruhusu kijana kwenda kwenye tukio lakini pale ambapo kunamakubaliano maalumu kama vile kwa kuondoka na kurudi katika muda ambao mlio kubaliana

Sema 'hapana' na 'samahani'

Wakati wazazi wanapotaka kusema 'hapana', inatakiwa iwe katika hali ya upole na heshima. Ita saidia pale wazazi watakapo elezea sababu husika za majadiliano yao. Kama wazazi wamefanya kosa semeni 'samahani' itasaidia kujenga mawasiliano mazuri na vijana.

Fundisha kwa mifano

Ni vizuri kuonyesha kwa vitendo kitu mbele ya vijana kuliko kuwambia maneno tu. Wakati mwingine wanaweza kujifanya hawajaelewa walicho elekezwa na wazazi lakini ujumbe wanakuwa wamepata. Kwa mfano kama unataka watoto wako wawe wapole na waangalifu, wafundishe na watu wengine katika njia ya upole na uangalifu.

Pia wazazi nao huhitaji msaada

Wakati mwingine huchoka na kuwaweza na kazi kuwa ngumu kuhusu vijana. Mzazi ongea na jamii au viongozi wa dini au wazazi wengine ambao wamepitia magumu kama yako inaweza kuwa msaada kwako. Pia inaweza kukusaidia kufikia malengo na kupata msaada kutoka familia zingine. Au wasiliana na namba ya simu ya huduma kwa wazazi kwa maoni zaidi au msaada: 1300 1300 52.



Kuwaacha watoto nyumbani katika hali yao



Wazazi wengi ambao wamehamia Australia huhitaji kujua ni umri gani ambao mtoto anakuwa huru na sheria inasemaje kuhusu kuwaacha watoto nyumbani.

Sheria katika NSW

Sheria katika NSW haijatoa ni umri gani ambao watoto wanaruhusiwa kuwa huru. Sheria inasema watoto wanatakiwa uangalizi na ulinzi juu ya hatari mbalimbali muda wote. Kama polisi wakiamini kuwa watoto hawa lindwi vizuri, huwaondoa watoto na kuwabadilishia wazazi au walezi kwa kosa la kuvunja sheria.

Wakati gani watoto wanaruhusiwa kuachwa nyumbani wenyewe?

Hutegemea na umri wao na upeo walionao, uwezo wao wakuweza kujilinda na kuishi kwa amani unapokuwa haupo. Watoto wanaoachwa nyumbani lazima wawe wanaufahamu wa kutosha na wenye uwezo wa kukabili matatizo ya gaffa na wenye kujuwa wanacho kifanya ni kipi na kujuwa wapi wanaweza kupata msaada.

Hakikisha watoto wanajua cha kufanya wakati wa dharura.

Hairuhusiwi kuacha watoto wachanga na watoto chipukizi pekeyao

Watoto wachanga na watoto chipukizi hawaruhusiwi kuwaachwa wenyewe sehemu yeyote ikiwemo nyumbani, kwenye gari au ndani ya treni. Si vizuri kuwaacha watoto hawa pekeyao hata kwa muda mfupi sababu hawezi kujilinda wenyewe au kuwa salama wenyewe. Hakikisha wewe au mtu yeyote unaye muamini yuko nao na wako salama.

Kwa muda gana utakuwa mbali nao?

Kama umepanga kuwaacha watoto wenyewe, unahitaji kufikiria umri wao na upeo wao, kwa muda wa siku ngapi na muda gani watakuwa wenyewe na wanaweza kujihudumia wakiwa wenyewe kwa huo muda utakao waacha? Sikuzote watoto wajue muda gani utatumia.

Mazingira hatarishi ya nyumbani ambayo yanaweza wazuru watoto ambao hawana uangalizi mzuri

Vitu hatari kwa watoto nyumbani ni hita, stovu, jiko la umeme, sehemu ya kuogea, kemikali, mabwawa ya kogelea, madirisha yaliyo wazi na milango yenye kujibamiza. Tovuti ya ulinzi wa mtoto itoayo taarifa ambayo inaweza kupunguza hatari za nyumbani kwa mtoto ni: www.kidsafensw.org.

Hakikisha watoto wanajua cha kufanya wakati wa dharura

Ongea nao namna ya kujilinda kama kutatokea dharula zifuatazo: moto, kubomoka kwa jengo, ajali au jeraha. Elekeza namna ya kupiga 000 wakati wa dharura. Hakikisha watoto wanajua namna ya kufungua kufuri za nyumbani wakati wa dharura. Usiwafungie watoto ndani wewe ukiwa nje.

Kuwaacha watoto wadogo wakiwa na watoto wakubwa

Kadri mtoto anavyokuwa hujifunza namna ya kujilinda na kulinda wengine. Ni kawaida kwa tamaduni nyingi watoto wakubwa kuwalinda watoto wadogo. Kama umemuacha mtoto mkubwa kuwatazama watoto wadogo unatakiwa kujua kuwa uliye muachia watoto hao anaupewa wa kutosha wa kuwalinda watoto hao dhidi ya hatari mbalimbali.

Waelekeze watoto namna ya kuwasiliana na wewe

Hakikisha watoto wanauwezo wa kuwasiliana na wewe na wanauwezo wa kutumia simu. Wapigie ili kujua kuwa kila kitu kinaenda vizuri. Unaweza kuiandaa familia nyingine au marafiki kuwa karibu nao wakati wewe haupo.



Namna yakuwa adabisha watoto nchini Australia

Kila sehemu wazazi watumie nidhamu kuwasaidia watoto kufanya mambo yaliyo sahihi kama vile, namna ya kujikinga na madhara mbalimbali, na namna ya kujituma. Jinsi wazazi wanavyo waadabisha watoto na sheria inayo husika na nidhamu hutofautiana nchi moja na nyingine. Nchini Australia kuna sheria zinazolinda watoto ambazo wazazi wote lazima wazifate.

Wazazi ambao ni wageni Australia wakati mwingine hushangaa sheria zinazo walinda watoto na zile ambazo zinazo waelekeza namna ya kuwalinda watoto. Kama wazazi wataelewa sheria hizo zitawajengea kujiamini kwa kuwaadabisha watoto wao bila kuvunja sheria.

Kuwachapa watoto ni uvunjanji wa sheria

Sheria katika NSW inasema:

- Wazazi hawaruhusiwi kuwachapa watoto sehemu ya kichwani au shingo;
- Si ruhusa kwa wazazi kuwachapa watoto sehemu yeyote ya mwili kwa kurudia rudia, kwa mfano kama itasababisha kuvimba;
- Mzazi anaruhusiwa kumchapa mtoto kwenye kiganja cha mkono. Hawatakiwi kumwadhibu mtoto kwa vifaa kama mkanda au fimbo.

Sheria inayolinda usalama wa watoto

Miili ya watoto ni rahisi kuharibiwa. Na adhabu inayoonekana ni ndogo kwa mkubwa inaweza kuleta madhara ya kudumu kwa mwili wa mtoto. Kichwani na shingoni ni sehemu hatari sana na inawezekana pigo dogo linaweza kuleta ulemavu au mtoto kuwa muoga sana. Kumtikisa mtoto kiholela ni hatari sana sababu inaweza pelekea mtikisiko wa ubongo na kusababisha ulemavu wa kudumu.

Kila sehemu wazazi watumie nidhamu kuwasaidia watoto kufanya mambo yaliyo sahihi kama vile, namna ya kujikinga na madhara mbalimbali, na namna ya kujituma.

Kipi wazazi wafanye

Matumizi ya adhabu za nguvu (mfano, kuchapa) kama aina ya adhabu inaweza kumuathiri mtoto kimwili na kiakili. Wazazi nchini Australia hushauriwa kutumia nidhamu ili kutotoa adhabu kubwa. Zifuatazo ni njia mahususi zitumikazo kuwaadabisha watoto pa bila kutoa adhabu kubwa.

Kanuni na zawadi

- Toa sheria ambayo ni sahihi na nyepesi kwa mtoto kuelewa.
- Hakikisha watoto wanaelewa kanuni, kwa nini umeziweka na namna wanaweza kuzitii.
- Toa zawadi kwa tabia nzuri kuwafanya watoto waendeleo kufanya mambo yanayo takiwa.

Adhabu inayoendana na umri [wa mtoto]

- Watoto chini ya miaka miwili huwa hawajui kanuni wala adhabu, kwahiyo kubadilisha tabia zao, huwaathiri na uondoa upeo wao katika kitu husika.
- Kuanzia umri wa miaka mitatu watoto wanaweza kujua kuwa matendo yao yana madhala: "Unapofanya hivi... ndicho hiki kitokeacho" Kwahiyo waeleze pale wanapofanya makosa.
- Kwa watoto zaidi ya miaka 2, 'mda wa kutoka nje' inaweza tumika, Waambie wakae sehemu moja kwa mda mfupi na fikiria sana tabia zao.

Watoto chipukizi na vijana

Kama kijana atashiriki mambo kama vile kutumia kompyuta kwa michezo au kuchati na marafiki anaweza kuacha kwa muda kidogo.

Wazazi nchini Australia hushauriwa kutumia nidhamu ili kutotoa adhabu kubwa.



Mawasiliano mazuri

- Usiwaambie watoto kuwa wao ni wabaya. Humfanya mtoto aendeleo kufanya mambo mabaya au makosa na kukosa kutojamini.
- Ongea na watoto huku ukiwa umewaadabisha kuhusu namna walivyo na kipi walicho jifunza.
- Kama watoto wataiga tabia mbaya wachukue sehemu tulivu na kisha waonye. Waambie wajiulize kwanini tabia zao si nzuri? na namna wanaweza kubadilika na kufanya mambo mazuri.
- Fundisha kwa mifano. Pale mtoto anapokuwa anafanya kosa, wasaidie namna ya kuondokana na tatizo hilo. Kwa mfano, kama mtoto huwa anaandika kwenye ukuta, mwambie afute na ikibidi msaidie.
- Usifoke unapokuwa unawaadabisha watoto. Jaribu kuhesabu mpaka 10 au pumua taratibu ukiwa unamuelekeza kwa upole.





Weka watoto salama

Australia ina sheria za kumlinda mtoto, kwahiyo wale wakubwa wakiwemo wazazi na wakubwa wengine ambao hulea watoto na vijana, lazima wazifuate sheria hizi kama vile unyanyaswaji wa watoto kimwili na kijinsia na utelekezaji watoto (chini ya miaka 18) ni kinyume cha sheria na anaweza adhibiwa.

Nini utelekezaji na unyanyasaji wa watoto?

Kutelekezwa maana yake wazazi au wakubwa kutomtimizia mtoto mahitaji muhimu kama vile makazi mazuri, chakula, elimu, nguo au matibabu. Pia kutowasimamia watoto na kuwaacha wapweke kwa muda mrefu.

Unyanyasaji wa kimwili maana yake mzazi au mlezi kuumumiza mtoto kwa kumchapa, kumsukuma sukuma. Si ruhusa kuwachapa watoto kwa vitu kama vile fimbo au mkanda katika kuwaadabisha. Ukeketaji nao ni unyanyasaji wa kimwili katika sheria za Australia na moja kwa moja muhusika hufungwa.

Unyanyasaji wa kiakili maana yake kuharibu hisia ya mtoto. Hii hutokea pale unapo waambia hawapendwi, kuwachukia mda wote, kuwatishia kuwapiga. Pia kumruhusu mtoto kutazama manyanyaso anayofanyiwa mtu katika familia, kama vile mama yao. Kwahiyo unyanyasaji wa akili ni mbaya kwa watoto na huwafanya wajihisi ni wanyonge.

Unyanyasaji wa kijinsia ni pale mtu anapomuingiza mtoto kwenye maswala ya kingono. Watoto huwa wanalazimishwa na kutishiwa ili wafanye kazi hii. Unyanyasaji wa kijinsia hupelekea dosari kwa watoto katika maisha yao.

Ndoa za utotoni na ndoa za kulazimishwa

Kuo au kuolewa chini ya miaka 18 ni kosa kisheria nchini Australia. Kuna baadhi ya matatizo huruhusu mtoto wa miaka 16 [au 17] kuo au kolewa lakini awe na kibali cha mahakama.

Pia ni kosa kumlazimisha mtu wa umri wowote kuo au kuolewa.

Ndoa za kulazimisha humfanya muhusika kutokuwa huru kwa sababu walimfokea, walimtisha au walimchochea.

Ni zipi alama za kunyanyaswa na kutelezwa?

Kutelekezwa – Mtoto ni mwepesi au mkonde kutokana na umri wake, wakati mwingine haogeshwi, hapewi chakula, anamatatizo ya kimwili na hapati msaada wowote, huwa ni vigumu sana kuelewa wakubwa.

Unyanyasaji wa mwili – Mtoto anakuwa na makovu kichwani, usoni au shingoni vidonda, kuchubuka au kukatwa, na kuvunjika au alama ya kukeketwa. Watoto walio nyanyaswa huwa wanagoma kuelezea yaliyo wasibu.

Unyanyasaji wa akili – Mtoto hujihisi yeye hana mafa, huwa hana imani na wengine, huwa na tabia mbaya na hajui namna ya kujichanganya na wenzake.

Unyanyasaji wa kijinsia – Wakati mwingine mtoto huelezea manyanyaso au hutoa alama isiyo nzuri, pia hupenda kudhulu mwili, huwa anagoma kula au hula kidogo na hupenda kulala na nguo zake. Anauwezo wa kuelezea matendo ya kimapenzi au ujuzi mkubwa kuhusu mapenzi kinyume na umri wao.

Australia ina sheria za kumlinda mtoto, kwahiyo wale wakubwa wakiwemo wazazi na wakubwa wengine ambao hulea watoto na vijana, lazima wazifuate sheria hizi.

Namna gani kutelekezwa kwa mtoto na unyanyasaji huripotiwa?

Mtu yeyote anaye dhani kuwa mtoto ametelekezwa, amenyanyaswa [kimwili], kijinsia au kiakili, au kumuingiza mtoto katika ndoa za utotoni au kumlazimisha aolewe unaweza kutoa taarifa kwenye Idara ya Familia & Huduma za Jamii (FACS) kwenye laini ya Child Protection kwa 132 111 (TTY 1800 212 936). Huwa ipo wazi masaa 24 kila siku, na siku saba za wiki. Kama muhusika hajui kingeleza wafanya kazi husika wataandaa mkarimani.

FACS itafanya nini?

Kama FACS inaamini kuna hatari katika kumtuza mtoto, wafanyakazi wake wataongea na wazazi pia na mtoto kama ana umri wa juu. Wanaweza kuongea na ndugu wa mtoto, mwalimu au walezi wowote. Mfanya kazi mwenyewe ataamua. Huduma za kijamii husaidia kuwalinda watoto na kuwaunganisha wazazi na huduma za misaada. Inapo gundulika mtoto yupo katika hatari na inapokuwa imetokea hivo FACS humuondoa mtoto katika familia zake na kumuweka katika eneo salama.

Kwa maelezo Zaidi

FACS ina tawi litwalo *Spot It; Help Stop It* Huonesha alama mahususi ya unyanyaswaji na utekelezaji. Hiki kitini hupatikana katika lugha tofauti. kama unataka kopi ya hiki kitini tembelea tovuti hii www.community.nsw.gov.au

Wapi pa kupata ushauri na msaada

Kuna huduma nyingi za kuwasaidia wazazi, watoto, vijana na familia. Miongoni mwa hizi kazi huduma zake ni bure. Wafanyakazi katika Halmashauri za mtaa, vituo vya afya husaidia familia kutafuta misaada ya karibu.

Huduma nyingi zimeorodheshwa hapo chini zitatumia mkalimani kwa wale wasio ongea kingereza.

Wafanyakazi katika Halmashauri za mtaa, vituo vya afya husaidia familia kutafuta misaada ya karibu.



Vituo Vidogovidogo Vya Afya

hutoa huduma kwa watoto, wazazi na familia. Ikiwemo kutembelea majumbani kwa wazazi wapya na watoto, huduma za makuzi ya watoto, makundi ya wazazi, kuongea na mshauri na ukaguzi wa afya za watoto.

Namba za simu za ushauri na msaada

ni namba za simu zitumiwazo kuongea na muhusika atakaye kusaidia. Baadhi ziko wazi masaa 24 na zingine siyo hivo. Huduma zote zinapatikana eidha kwa gharama au bure, gharama pale unapotumia mawasiliano kwa kutumia simu za mezani.

- **Namba za simu kuhusu mzazi** – mshauri mzoefu atasikiliza na kutoa msaada unaohitajika na atatoa taarifa kuhusu, tabia za watoto, nidhamu, makuzi, wazazi wa aina moja, habari za shuleni na uangalizi wa mtoto.
Simu: 1300 1300 52
www.parentline.org.au
- **Tresillian Parent's Help Line** – manesi wanao husika na watoto pamoja na familia watakupa ushauri kuhusu kuwatunza watoto mpaka umri wa miaka 5.
Simu: 1800 637 357 au (02) 9787 0855
www.tresillian.net
- **Karitane Careline** – Manesi wanaohusika na familia watatoa ushauri kuhusu ujauzito na malezi ya watoto mpaka umri wa miaka 5.
Simu: 1300 227 464
www.karitane.com.au
- **Namba za simu za ushauri wa mahusiano ya kifamilia** – Hutoa ushauri kuhusu parenting na mikakati baada ya kutengana.
Simu: 1800 050 321
www.familyrelationships.gov.au
- **Namba za simu juu ya manyanyaso ya wafanyakazi wa ndani** – Hutoa ushauri na taarifa kuhusu matatizo ya kifamilia. Wafanyakazi mashuhuri wenye uzoefu wa kazi za ndani watakuhudumia.
Simu: 1800 656 463
(TTY 1800 671 442)
- **Mawasiliano kuhusu kumlinda mtoto** – Kama umegundua mtoto ananyanyaswa au ametelekezwa.
Simu: 132 111 (TTY 1800 212 936).
- **Mawasiliano kuhusu kumsaidia mtoto** – Ukipiga utapata ushauri wa bure unaohusu watoto kuanzia miaka 5 na 25.
Simu: 1800 55 1800
- **Mawasiliano kuhusu maisha** – Kama mtu ana wasiwasi wowote wa kimaisha piga namba hii.
Simu: 13 11 14
www.lifeline.org.au

Taarifa za Wazazi

Hizi tovuti hutoa taarifa kuhusu shughuli za wazazi, watoto na familia.

- Resourcing Parents kwenye: www.resourcingparents.nsw.gov.au
- NSW Department of Family Community Services kwenye: www.community.nsw.gov.au
- Families NSW kwenye: www.families.nsw.gov.au
- Raising Children Network kwenye: www.raisingchildren.net.au

Vituo vya Taarifa kwa Wahamiaji (MRCs)

MRCs Hutoa huduma kwa wahamiaji na wakimbizi. Kama zifuatazo: msaada wa makazi, mawasiliano, rufaa, msaada wa kifamilia, msaada wa vikundi, mikakati ya wazazi, huduma za kusaidia walemavu, mikakati ya kusaidia uvujaji sheria kwa wafanyakazi wakazi za ndani, mikakati ya kijamii na taarifa za lugha mbalimbali. Kama unahitaji msaada kwa yaliyotajwa hapo juu wasiliana na MRC Ndani ya eneo lako.

Auburn Diversity Services

17 Macquarie Road
Auburn NSW 2144
Simu: (02) 9649 6955
Barua pepe: info@auburndiversity.org.au
www.auburndiversity.org.au

Community MRC

4 /1 Horwood Place
Parramatta NSW 2150
Simu: (02) 9687 9901
Barua pepe: cso@cmrc.com.au
www.cmrc.com.au

Fairfield Migrant Resource Centre

Corner Railway Parade and
McBurney Road
Cabramatta NSW 2166
Simu: (02) 9727 0477
Barua pepe: info@fmrc.net
www.fmrc.net

Illawarra Multicultural Services

17 Auburn Street
Wollongong NSW 2500
Simu: (02) 4229 6855
Barua pepe: info@ims.org.au
www.ims.org.au

Liverpool MRC

Ground floor, 108 Moore Street
Liverpool NSW 2170
Simu: (02) 9601 3788
Barua pepe: info@lmrc.org.au
www.lmrc.org.au

Macarthur Diversity Services

Level 3, Suite 2,
Campbelltown City Centre
171-179 Queen Street
Campbelltown NSW 2560
Simu: (02) 4627 1188
Barua pepe: info@mdsi.org.au
www.mdsi.org.au

Metro Assist

Level 2, 59-63 Evaline Street
Campsie NSW 2194
Simu: (02) 9789 3744
Barua pepe: metromrc@metromrc.org.au
www.metromrc.org.au

Northern Settlement Services

8 Chaucer Street
Hamilton NSW 2303
Simu: (02) 4969 3399
Barua pepe: nss@nssservices.com.au
www.nssservices.com.au

St George MRC

552 Princes Highway
Rockdale NSW 2216
Simu: (02) 9597 5455
Barua pepe: sgmrc@sgmrc.org.au
www.sgmrc.org.au

Sydney Multicultural Community Services

3 General Bridges Crescent
Daceyville NSW 2032
Simu: (02) 9663 3922
Barua pepe: info@sydneyemcs.org.au
www.sydneyemcs.org.au

SydWest Multicultural Services

Level 2/125 Main Street
Blacktown NSW 2148
Simu: (02) 9621 6633
Barua pepe: info@sydwestmsi.org.au
www.sydwestmsi.org.au

Huduma za Ushauri kwa Wakimbizi

NSW Service for the Treatment and Rehabilitation of Torture and Trauma Survivors (STARTTS)

Husaidia watoto na wakubwa ambao walisha pata mateso, vita, unyanyasaji auwalikosa haki za kibinadamu kabla ya kuja Australia na wanahitaji msaada ili wawe na amani na hali yao iwe kama zamani.
Simu: (02) 9794 1900
www.startts.org.au

Transcultural Mental Health Centre

Husaidia watu ambao wanamatatizo ya akili walio toka katika tamaduni tofauti na lugha tofauti. Kama unahitaji huduma zinazo husika na ushauri na taarifa ya afya ya akili.
Simu: 1800 648 911 au (02) 9912 3851
www.dhi.health.nsw.gov.au

Maandishi

